

02.04.2026

TANGAZO LA ZABUNI YA UGAVI WA KATANI- KUDU (SISAL TWINE) MSIMU 2026/2027

Zabuni na: KCU/G/2026/2027/05

1. KCU (1990) Ltd Inatangaza zabuni ya kuuziwa Katani-Kudu (Sisal Twine) 204 kwa ajili ya kufungia magunia yenye kahawa yanaposafirishwa kutoka kwenye Vyama vya Ushirika vya Msingi kuletwa kwenye kiwanda cha kukobolewa kahawa msimu 2026/2027.
2. Kudu moja iwe na uzito wa kilo moja.
3. Mwombaji aeleze ni muda gani anaweza kuleta kudu baada ya kupewa agizo (Order/LPO).
4. Mwombaji ataje bei atakayo toza kwa kudu moja, mpaka zinapofikishwa kwenye ghala la KCU (1990) Ltd. (Bei ieleze kama ni pamoja na VAT au bila VAT)
5. Ombi la zabuni liwe na jina na anwani halisi ya mwombaji, aidha aoneshe mahali Ofisi ilipo (Physical address)
6. Maombi yaambatane na ada ya TShs. 100,000/= ambazo hazitarejeshwa kwa mwombaji. Fedha hizo zilipwe kupitia A/C Namba **01J1055955002General A/C**
7. Tathmini itafanywa kwa kuzingatia vigezo 2-6 vilivyo tajwa hapo juu.
8. Bahasha ya ifungwe vizuri kwa lakiri na kuandikwa juu yake:- **"MAOMBI YA ZABUNI YA UGAVI WA KATANI- KUDU (SISAL TWINE) MSIMU 2026/2027."** kwa anwani tajwa hapa chini,

MENEJA MKUU,
KCU (1990) LTD,
P.O BOX 5,
BUKOBA.

9. Bahasha hiyo iletwe kwa mkono katika Ofisi ya Manunuzi KCU kabla au mnamo tarehe 20.4.2026 saa 4.00 asubuhi siku ya Jumatatu na ufunguzi wa maombi yote utafanyika muda huo, waombaji au wawakilishi wa waombaji wanaalikwa katika sherehe ufunguzi mara tu baada ya saa ya mwisho yakupokea zabuni.
10. Maombi yatakayochelewa, maombi yasiyokamilika, maombi yaliyowasilishwa kwa njia ya kieletroniki na maombi yasiyokuwepo siku ya ufunguzi hayatahusishwa na uchambuzi wa kumpata mzabuni.

Imetolewa na;

MENEJA MKUU
KCU (1990) LTD

